

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



14 JUNI, 2016



# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA AROBAINI NA MBILI – 14 JUNI, 2016

### I. MASWALI:

#### OFISI YA WAZIRI MKUU:

##### 354. MHESHIMIWA HAWA MCHAFU CHAKOMA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Moja ya tatizo kubwa nchini ni ukosefu wa ajira kwa vijana, Serikali imeweka vipaumbele vyatia kuanzisha na kukuza viwanda vidogo, vyatia katika na vikubwa kwa lengo la kuajiri vijana wengi wa Kitanzania:-

Je, Serikali ina mikakati ipi ya kuhakikisha azma hiyo njema inafikiwa.

##### 355. MHESHIMIWA GODBLESS JONATHAN LEMA (ARUSHA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Hivi karibuni Mhe. Rais ameamuru Wakuu wa Mikoa kuwakamata na kuwaweka mahabusu vijana watakaokutwa wanacheza *pool table* na *draft* mitaani kama ishara ya mizaha katika nguvu kazi:-

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa kutengeneza ajira ili vijana waweze kuajiriwa na kuepuka adhabu hiyo itakayotekelizwa na Wakuu wa Mikoa;
- (b) Ni dhahiri kwamba Taifa letu linapita katika adhabu kubwa ya umaskini. Je, Serikali haioni kwamba Taifa linaweza kuingia katika vurugu kubwa kati ya vijana wasiokuwa na ajira na Jeshi la Polisi.

#### **OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

#### **356. MHESHIMIWA SOPHIA HEBRON MWAKAGENDA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Shule ya Sekondari ya Ndembela Wilayani Rungwe awali ilijengwa kwa nguvu za Wananchi na baadaye Kanisa la Waadventista Wasabato liliingia kama wabia na kuiendeleza na hatimaye kuiendesha Shule hiyo ikiwa na majengo yaliyokamilika; baada ya Wananchi kuihitaji Shule yao, Kanisa limekubali kuirejesha kwa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe kwa fidia ya shilingi 947,862,000 Halmashauri imeomba Wizara ya Elimu isaidie kulipa fidia hiyo:-

Je, ni lini Serikali itasaidia kuirejesha Shule hiyo mikononi mwa Wananchi kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe.

## **WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

### **357. MHESHIMIWA NJALU DAUDI SILANGA (ITILIMA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:- Mhe. Rais kwenye Kampeni za Uchaguzi aliahidi kupanua mpaka wa *Game Reserve* iliyoko Maswa:-

Je, ni lini ahadi hiyo itatekelezwa.

### **358. MHESHIMIWA AUGUSTINO MANYANDA MASELE (MOGWEE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:- Sekta ya Utalii ina mchango mkubwa katika kuliingizia Taifa fedha za kigeni:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha miundombinu ya Barabara, Hoteli na *Airstrips* katika Pori la Akiba la Kigosi ili kuweza kuvutia Watalii wengi zaidi kutembelea vivutio vilivyopo katika Pori hili zuri la Kigosi na Muyowosi.

## **WIZARA YA NISHATI NA MADINI:**

### **359. MHESHIMIWA DAIMU IDDI MPAKATE (TUNDURU KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:- Katika Wilaya ya Tunduru iko miradi mingi ya REA ambayo Kampuni mbili zimepewa kazi hiyo lakini Wakandarasi wanausua kukamilisha miradi hiyo na muda wake umeisha kwa kigezo cha kutolipwa:-

Je, ni lini Serikali itatoa pesa kukamilisha miradi hiyo.

## **WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

### **360. MHESHIMIWA HAMADI SALIM MAALIM (KOJANI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Jeshi la Polisi ni chombo muhimu kinacholinda usalama wa raia na mali zao. Askari hawa wanapomaliza mafunzo yao kwa ngazi mbalimbali kama vile Sajenti, Staff Sajenti, Meja na nyingine, hucheleweshwa sana kulipwa maslahi yanayoendana na vyeo vyao:-

Je, ni kwa nini Askari hao hawalipwi kwa wakati.

## **WIZARA YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:**

### **361. MHESHIMIWA MWANNE ISMAEL MCHEMBA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi:- Wakulima wa Tumbaku wamekuwa wakilipwa kwa dola pindi wanapouza mazao yao:-

- (a) Je, nani huwapigia hesabu za kitaalamu;
- (b) Je, Wakulima wote wamefunguliwa akaunti Benki.

## **WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:**

### **362. MHESHIMIWA HAWA ABDULRAHMAN GHASIA (MTWARA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji:- Halmashauri za Mkoa wa Mtwara kwa kushirikiana na Kampuni ya HELM wanakusudia kujenga kiwanda cha mbolea huko Msanga Mkuu – Mtwara Vijijini:-

Je, ni lini Serikali itaridhia mradi huo kuanza.

### **363. MHESHIMIWA STEPHEN JULIUS MASELE (SHINYANGA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji:-

Je, ni lini Serikali itataifisha Kiwanda cha Nyama Shinyanga Mjini baada ya Mwekezaji kushindwa kukiendesha.

#### **II. HOJA ZA SERIKALI:**

##### **WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Kwamba, Bunge likubali kujadili Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2015 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

Kwamba, Bunge likubali kupitisha Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

*(Majadiliano yanaendelea)*

**DODOMA**  
**14 JUNI, 2016**

**DKT. T. D. KASHILILAH**  
**KATIBU WA BUNGE**